
CBT

Co-operative Bank



# MKUTANO MKUU WA

## KWANZA WA WANACHAMA WA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA LIMITED (CBT)

**HATUA MOJA, MBELE ZAIDI**

17 OKTOBA 2024

DODOMA


coop.
BANK


-OPERATIVE BANK OF TANZANIA
OMA BRANCH
ATM

# Yaliyomo


Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mkutano 13

Kuthibitisha Akidi 13

Kufungua Mkutano 13

Kuafiki Dondoo Za Mkutano 13

Uwasilishaji wa Cheti cha Usajili cha Co-Operative Bank Of Tanzania Limited. 15

Wasilisho la Mpango Mkakati wa Co-Operative Bank Of Tanzania Limited 17

Kupitisha Katiba (Memarts) ya Co-Operative Bank Of Tanzania Limited 40

Kujadili na Kupitisha Muundo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Vyama vya Ushirika. 47

Kuidhinisha Thamani na Mgawanyo wa Hisa kwa Wanahisa Waanzilishi wa Co-Operative Bank Of Tanzania Limited. 52

Kudhinisha ukomo wa Madeni kwa Mwaka 2024 56

Kuidhinisha Mkaguzi wa Hesabu kwa Mwaka 2024/2025 59

Kupokea Mali na Madeni kutoka Kilimanjaro Co-Operative Bank Limited (Kcbl) na Tandahimba Cooperative Bank Limited (Tcbl) 64

Kuidhinisha kuhamisha Mali na Madeni Kutoka Chama Kwenda Kampuni. 66

Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi ya Co-Operative Bank of Tanzania 66

Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti 69

Kufunga Mkutano 69

# Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wanachama

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Wanachama na Wanahisa wa Co-operative Bank of Tanzania Limited (CBT) utafanyika siku ya Alhamisi ya tarehe 17 Octoba, 2024 kwenye Ukumbi wa Generation jijini Dodoma (eneo la Kisasa), kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi kujadili dondoo zifuatazo:

1. Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mkutano.
2. Kuthibitisha Akidi.
3. Kufungua Mkutano.
4. Kuafiki Dondoo za Mkutano.
5. Uwasilishaji wa Cheti cha Usajili cha Co-operative Bank of Tanzania Limited.-
6. Wasilisho la Mpango Mkakati wa Co-operative Bank of Tanzania Limited.
7. Kupitisha Katiba (MEMARTS) ya Co-operative Bank of Tanzania Limited.
8. Kujadili na kupitisha Muundo wa usimamizi wa uwekezaji wa vyama vya Ushirika.
9. Kuidhinisha thamani na mgawanyo wa hisa kwa wanahisa waanzilishi wa Co-operative Bank of Tanzania Limited.
10. Kuidhinisha ukomo wa madeni kwa mwaka 2024.
11. Kuidhinisha Mkaguzi wa Hesabu kwa mwaka 2024.
12. Kupokea mali na madeni kutoka Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) na Tandahimba Cooperative Bank Limited (TCBL).
13. Kuidhinisha kuhamisha mali na madeni kutoka Chama kwenda kampuni.
14. Azimio maalum la uchaguzi wa wajumbe huru wa Bodi ya Co-operative Bank of Tanzania Limited.
15. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
16. Kufunga Mkutano.

**MAELEZO**

1. Makabrasha ya Mkutano yatapatikana katika Benki ya Ushirika Kilimanjaro jijini Moshi na Benki ya Ushirika Tandahimba, Makao Makuu ya Benki ya Ushirika Dodoma na kwenye ukumbi wa Generation uliopo maeneo ya Kisasa, Dodoma siku ya Mkutano.
2. Wanachama na Wanahisa watakaoshindwa kuhudhuria wana haki ya kutuma mwakilishi.
3. Wanachama na Wanahisa watakao hudhuria Mkutano watajigharamia usafiri na malazi.
4. Chama/Taasisi/Kampuni kinaombwa kutuma mjumbe mmoja tu kuhudhuria Mkutano.

**Kwa mawasiliano na maelezo zaidi tafadhali tumia anuani zifuatazo:**

Mkurugenzi Mtendaji,
Co-operative Bank of Tanzania Limited,
S.L.P 201,
DODOMA.

KWA IDHINI YA BODI

...........................
John B. Rugambo
**Katibu wa Bodi**

## Taarifa ya Mwenyekiti



> "Ushirika... Pamoja tujenge Uchumi Imara na Endelevu.
>
> Hatua Moja... Mbele Zaidi.

**UTANGULIZI**

**Ndugu Wanahisa na viongozi wenzangu,**

Kwa niaba ya viongozi wenzangu na wakurugenzi wa Bodi wenye dhamana ya kusimamia benki ya Ushirika Tanzania - CBT, ninayo furaha kuwakaribisha wote katika Mkutano Mkuu wa kwanza wa wanahisa wa Co-operative Bank of Tanzania (CBT). Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutujalia kukutana tena kwa pamoja. Pili nimshukuru sana kwa niaba ya wanahisa, bodi na wafanyakazi wetu wote Mhe. Hussein Mohamed Bashe - Waziri wa Kilimo kwa kujali na kutoa muda wake kufungua Mkutano wetu Mkuu wa Kihistoria. Ahsante sana. Aidha niwashukuru ninyi wanahisa wote kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu, kwa wingi.

Ndugu Wanahisa, naomba pia kuwashukuru na kuwatambua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ninayoiongoza, nikishirikiana na wenzangu wanne akiwemo Bw. Mohamed Nassoro Mwinguku (Makamu Mwenyekiti), Bi. Chiku Issa, Prof. Faustine Bee – (Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi na Udhibiti Vihatarishi), CPA. Dkt. Veronica Nyahende (Mjumbe), CPA. Mwamini Mussa (Mjumbe), Bi. Mariam Said Mwanzalima (Mjumbe), Bw. Fredrick Nshekanabo (Mjumbe), Bw. Denis Mwoleka (Mjumbe), Dk. Rashid Adam Tamatamah (Mjumbe), Bw. John Baptiste Rugambo (Katibu wa Benki). Wajumbe hawa wa Bodi wameonesha umahiri, uzoefu na weledi mkubwa katika kusimamia mchakato wa uanzishwaji wa Co-operative Bank of Tanzania (CBT). Wamehakikisha tunarejesha taswira na mahusiano chanya na wateja wetu, wadau, Serikali na jamii kwa ujumla na kwa kushirikiana na Menejimenti wamefanikisha mageuzi makubwa kwa Benki yetu kufikia hatua hii. Kipekee tunaipongeze Menejimenti na Watumishi wetu wote chini ya uongozi madhubuti wa Mkurugenzi Mkuu kwa maono na uthabiti, ndugu Godfrey Ng'urah. Hongera sana Mkurugenzi Mkuu na timu yako kwa kazi kubwa na mageuzi makubwa.

**USIMAMIZI NA UTAWALA BORA**

**Co-operative Bank of Tanzania (CBT)** itaendelea kuimarisha usimamizi, udhibiti, ueledi na uwazi katika utendaji wa Benki kwa kuhakikisha uwepo wa mifumo, sera na miongozo ya utawala bora na kuhakikisha yafuatayo yanatekelezeka:-

1) Vikao vya usimamizi kila robo vya Bodi na kila mwezi kwa menejimenti;
2) Kuchapisha kila Robo, matokeo ya fedha na utendaji wa Benki;
3) Vikao vya kila Robo vya Kamati ya Bodi ya Ukaguzi na udhibiti vihatarishi;
4) Kusimamia utekelezaji kikamilifu mkakati na dira kuu ya Benki ya miaka mitano - 2025-2029
5) Uandaaji na uidhinishaji wa sera na miongozo mipya ya kiutawala na usimamizi wa Benki;

6) Kuongoza Benki kwa misingi na sera za utawala bora na uwazi
7) Mageuzi ya kimkakati na uendeshaji na kufanikisha mtaji na usajili wa Benki ya Ushirika Tanzania
8) Kuimaraisha Weledi na kuthibiti vihatarishi ndani ya Benki;

**Co-operative Bank Of Tanzania (CBT)**
Mnano Mei 26, 2024, Benki ya KCBL na TCBL ziliunganishwa pamoja na kusajiliwa na Mrajisi na baadae kupewa leseni ya mpito na BOT mnamo tarehe 23/07/2024 kama Benki mpya inayojulikana kama Co-operative Bank of Tanzania Limited (CBT). Benki hii inamilikiwa na Wanaushirika kwa 51% na Taasis , Makampuni na Watubinafsi 49%. Makao makuu ya CBT yatakuwa Dodoma pamoja na tawi la benki. Ukarabati na Makao makuu na tawi tayari umeshakamilika tayari kwakuanza kutumika kutoa huduma. Aidha mnamo tarehe 30/09/2024 Benki ilifanikwa kuunganisha mfumo mkuu wa Benki na kuanza kufanya kazi kama Co-operative Bank of Tanzania (CBT) kuanzia tarehe 01/10/2024.

Benki ya Ushirika Tanzania inatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni kulingana na ratiba ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**HITIMISHO**

Kwa niaba ya viongozi wenzangu katika Bodi, nirudie tena kuwashukuru sana Wanahisa, Menejimenti ya Benki yetu, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, na wafanyakazi wote wa Benki kwa kuonyesha umahiri, weledi, kujitoa na kufanya kazi kwa matokeo chanya.

Niwashukuru wanahisa na wajumbe wote, kwa kuhudhuria mkutano wetu mkuu wa kwanza wa kihistoria tukiwa na Benki mpya ya Ushirika, kwa wingi hivi. Niwashukuru pia kwa dhamira yenu ya dhati kuwekeza na kujenga Benki mpya, bora na ya kisasa- Co-operative Bank of Tanzania (CBT). Niombe Vyama vya Ushirika viendelee kuwekeza. Vilevile niombe Vyama vya Ushirika na Wadau kuanza kutumia Benki hii mpya kwa huduma bora na za kiubunifu zaidi.

Aidha, nimshukuru kwa dhati muwekezaji wetu wa kimkakati, Benki ya CRDB kwa kutushika mkono kweli kweli mpaka hapa. Tunawashukuru sana kwa kusamehe mtaji mlio toa na kulipia hasara zote za Benki zote mbili, kwa kweli tusingeweza bila ninyi. Mkurugenzi Mkuu wa CRDB na Mwenyekiti wa Bodi tunawashukuru sana sana.

Kipekee nitambue pia na kuishukuru Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC), Wadau na wateja wetu wote kwa kutuunga mkono, kufanikisha dhamira ya mageuzi ya Benki zetu kuwa Co-operative Bank of Tanzania (CBT) ili kusaidia vyama vya ushirika hapa nchini na sekta mtambuka kujiendesha kibiashara na kuleta ujumuishi wa kifedha na ustawi kwa wote.

Hatua Moja, Mbele Zaidi.

..........................
Prof. Gervas Machimu
Mwenyekiti wa Bodi



# WASIFU WA  WAJUMBE WA BODI



**Prof. GERVAS MATHIAS MACHIMU**
Mwenyekiti wa Bodi

Prof. Gervas Machimu ni Profesa Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo anafundisha kozi za maendeleo vijijini. Pia anahudumu kama Mkurugenzi - Taasisi ya Elimu Endelevu ya Ushirika – (MoCU). Prof. Gervas Machimu amefanya kazi mbalimbali za ushauri na huduma za jamii.

Prof. Gervas Machimu ana Shahada ya uzamivu katika Maendeleo vijijini (Dec. 2012 hadi Nov. 2016); shahada ya uzamili katika Maendeleo Vijijini (2005 hadi 2007) Hkauntoovkear &ChTuykoe Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) mkoani Morogoro, Tanzania; Diploma ya Uzamili katika Uchambuzi wa Umasikini (Mei 2010 hadi Juni 2011) kutoka Chuo Kikuu cha Erasmus Rotterdam nchini Uholanzi; Shahada ya Falsafa (2000 hadi 2004) Chuo Kikuu cha Pontifical Urbaniana Roma, Italia.

Kati ya mwaka 2018 na 2021, alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Akiba na Mikopo Wazalendo na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT 1992 Ltd).

# Wasifu wa Wajumbe wa Bodi



**Mohamed Nassoro Mwinguku**
Makamu Mwenyekiti wa Bodi

Bw. Mohamed Nassoro Mwinguku ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tandahimba Community Bank Plc. Bw. Mohamed Nassoro Mwinguku pia ni Meneja Mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika, TANECU. Kabla ya nyadhifa zake hizi kwa sasa, alikuwa Katibu Mkuu wa shirika lisilo la kiserikali la Mtwara AIDS, Katibu Mkuu wa kitengo cha utunzaji na kujumlisha mizigo bandari ya Mtwara. Ni msomi katika Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara katika Fedha kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA).



**Mariam Said Mwanzalima**
Mjumbe wa Bodi

Bi. Mariam Said Mwanzalima ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Tandahimba Community Bank Plc na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba. Ni mbobezi mwenye uzoefu wa miaka zaidi ya Ishirini katika maswala ya Utawala wa Umma. Amehudumu kama Mjumbe wa Kamati ya Leseni za Biashara katika Wizara ya Viwanda na Biashara na Mjumbe Kamati ya Tehama katika maandalizi ya mpango wa mageuzi ya uhamiaji. Ana Shahada ya uzamili katika utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe Tanzania.



**Fredrick Nshekanabo**
Mjumbe wa Bodi

Bw. Fredrick Nshekanabo ni Afisa Mkuu wa Fedha kutoka Benki ya CRDB Bank Plc. Fredrick alianza kazi CRDB, Februari22 – 1999. Kabla ya wadhifa wake wa sasa, alikuwa Meneja wa huduma wa fedha. Mhasibu Daraja la kwanza (I) na Afisa wa benki ya CRDB. Ni msomi mwenye CPA (T), shahada ya Sayansi ya Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Strathclyde, UK na Stashahada ya Juu ya Uhasibu kutoka chuo cha utawala wa fedha (IFM), Dar es Salaam.



**Denis Mwoleka**
Mjumbe wa Bodi

Bw. Denis Mwoleka ni Meneja wa kanda ya kusini kutoka Benki ya CRDB Bank plc alianza kazi CRDB Mwaka 2006. Bw. Denis amehudumu pia kama Meneja wa Matawi Mbalimbali katika Benki ya CRDB kabla ya kuwa Meneja wa Kanda akianzia kanda ya Nyanda za juu na sasa kanda ya kusini.

Bw. Denis ni msomi mwenye cheti kinachotambuliwa na Bodi ya Uhasibu Tanzania CPA (T), Cheti cha usimamizi wa nyezo na pia anashahada ya Masoko kutoka chuo kikuu cha Iringa.



**Dr. Rashid Adam Tamatamah**
Mjumbe wa Bodi

Dk. Rashid Adam Tamatamah ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwenye Shahada ya Uzamili ya Kilimo cha Majini na Usimamizi wa Uvuvi na Shahada ya Uzamivu ya Limnolojia. Alipata mafunzo nchini Tanzania, Scotland (Uingereza) na Canada. Dk. Tamatamah ana uzoefu wa zaidi ya miaka thelathini (30) wa kutoa mafunzo ya uvuvi na kufanya tafiti na ushauri katika masuala ya uvuvi na mazingira . Amewahi kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi katika mashirika 7 tofauti. Kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2018 alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kabla ya kuteuliwa kushika nafasi ya Katibu Mkuu wa Uvuvi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wadhifa alioutumikia kati ya Julai 2018 hadi Februari 2023.



**John Baptiste Rugambo**
Katibu wa Benki

Bw. John Baptiste Rugambo ni Katibu wa Benki mbobevu mwenye uzoefu wa miaka zaidi ya 20. Amefanya kazi katika benki ya CRDB Bank Plc tangu mwaka 1999 na kukua katika ufanisi wa kazi zake mpaka kufikia nafasi hii aliyopo sasa. Amehudumu nafasi ya ukatibu wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Wananchi Tandahimba tangu mwaka 2015.

Kabla ya kuwa katibu wa benki ya CRDB, Bw. Rugambo alifanya kazi katika nafasi mbalimbali katika benki ya CRDB, ikiwemo nafasi ya Mkurugenzi wa Masoko na Utafiti, Meneja Masoko, Meneja Mradi wa Tembo card na Meneja wateja wa Taasisi. Kabla ya kujiunga na CRDB, Bw. Rugambo alifanya kazi Citibank kama Mkuu wa Huduma kwa wateja na Afisa Mahusiano Taasisi za Kifedha. Amehudumu pia kama Mshauri wa Bodi ya AIESEC Tanzania na ni mjumbe mwanzilishi wa Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania amabapo alihudumu mwanzo kama Makamu Mwenyekiti na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo. Ana shahada ya uzamili ya Usimamizi wa Biashara wa Kimataifa na shahada ya kwanza ya Usimamizi wa Biashara wa Kimataifa kutoka Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Marekani cha Afrika (USIU) mjini Nairobi, akibobea kwenye Masoko. Pia amefuzu programu ya Watendaji Wakuu katika Chuo cha Biashara cha London

# Wajumbe wa Bodi wa Benki ya CBT



**BI. CHIKU ATHMAN ISSA**
Mjumbe wa Bodi

Bi. Chiku Issa ana uzoefu wa zaidi ya miaka 30 katika sekta ya benki, katika biashara usimamizi wa wateja wadogowadogo, wa kati na wakubwa. Alifanya kazi kama Meneja wa Kanda ya Kaskazini wa benki ya CRDB, alifanya kazi pia kama Meneja wa Tawi la Arusha, ambapo alihamasisha ukuaji wa wafanyabiashara wadogo, mikopo katika mnyororo wa thamani wa kilimo na upatikanaji wa fedha za wanawake. Kabla ya kujiunga na CRDB, alifanya kazi katika ofisi ya Waziri Mkuu kama Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo alihamasisha harakati za ushirika katika mkoa huo.

Bi. Chiku Issa ana shahada ya uzamilCiokatika usimamizi wa Biashara, Diploma ya Maendeleo ya Uhasibu kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. Pia amehudhuria mafunzo mbalimbali ya uongozi na biashara.

Pia ni Mjumbe wa Bodi ya Hospitali ya Mount Meru iliyopo jijini Arusha, Shule ya Sekondari ya Visitation na amehudumu katika Bodi mbalimbali zaidi ya 10 za Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Serikali kwa kipindi cha miaka 15 iliyopita.



**PROF. FAUSTINE KARRANI BEE**
Mjumbe wa Bodi

Prof. Faustine Karrani Bee ni Profesa wa mafunzo ya maendeleo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) – Morogoro, tangu Agosti 2022. Kuanzia Machi, 2019 hadi Julai, 2022, Prof. Bee alikuwa Profesa wa mafunzo ya Maendeleo na pia alihudumu kama Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Kabla ya kuteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Prof. Bee alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), ambapo pia alikuwa Profesa wa Maendeleo ya Uchumi. Prof. Bee ana shahada ya Udaktari na shahada ya uzamili katika masomo ya maendeleo, pamoja na shahada ya kwanza katika uchumi.

Prof. Bee anawakilisha Bodi ya CRDB kwenye Bodi ya KCBL, ambapo CRDB ni mwekezaji wa kimkakati katika benki ya KCBL. Prof. Bee alihudumu katika Bodi ya CRDB kuanzia 2018 hadi 2021 na alichaguliwa tena kwa muhula wa pili (2021 – 2024). Prof. Bee ni mjumbe wa Kamati ya Mikopo na Kamati ya Utawala, Uteuzi na Rasilimali Watu ya Bodi ya benki ya CRDB.

# Wajumbe wa Bodi wa Benki ya CBT



**DKT. VERONICA ROBERT NYAHENDE**
Mjumbe wa Bodi

Dkt. Veronica Robert Nyahende ni Mkurugenzi wa Fedha na Mipango katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbli (MOI) nchini Tanzania. Dkt. Veronica ana MBA (Finance) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni mhitimu kutoka Taasisi ya Uhasibu Arusha (ADA) – Tanzania, pia ni mwanachama aliyesajiliwa na NBAA kama mhasibu wa umma aliyethibitishwa nchini Tanzania [ACPA (T).

Ana shahada ya uzamivu katika Usimamizi (Financial Management) kutoka Chuo Kikuu cha Fedha na Uchumi cha Dongbei (Jamhuri ya China), pia ni mwanachama aliyethibitiHshawnoaver &na Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania (IODT) katikva ngazi ya Umahiri. Dkt. Veronica pia amehudumu katika Kamati mbalimbali za Bodi ikiwemo ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Chuo Kikuu cha Ardhi.

Dkt. Veronic ana uzoefu katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya Mawasiliano, Usimamizi wa Fedha, Benki, Uhasibu, Ukaguzi, Rasilimali Watu, Utawala, Mipango na Utafiti



**CPA MWAMINI JAFARI MUSSA**
Mjumbe wa Bodi

CPA Mwamini ni meneja wa fedha katika Maamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania - Kiwanja cha ndege cha KIA. CPA Mwamini ana shahada ya uzamili ya Sayansi (MSc) katika fedha na uwekezaji. Vilevile CPA Mwamini ni mwanachama aliyesajiliwa na NBAA kama mhasibu wa umma aliyethibitishwa nchini Tanzania CPA(T). CPA Mwamini kwa sasa anahudumu kama mjumbe wa bodi ya Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) na mjumbe wa bodi katika KIA SACCOS Ltd

## Dondoo Na. 1

### UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MKUTANO

Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mkutano

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Kwanza wa Co-operative Bank of Tanzania ili kuongoza Mkutano kama ulivyoainishwa kwenye Notisi.

## Dondoo Na. 2

### KUTHIBITISHA AKIDI

Kwa mujibu wa kanuni, akidi ya Mkutano wa Wanachama wa Co-operative Bank of Tanzania inapaswa kulenga katika kufikia maridhiano na idadi inayotakiwa ni Wanachama Mia Moja (100) au idadi isiyopungua nusu ya wajumbe wote.

## Dondoo Na. 3

### KUFUNGUA MKUTANO

Kwa mujibu wa kanuni, akidi ya Mkutano wa Wanachama wa Co-operative Bank of Tanzania inapaswa kulenga katika kufikia maridhiano na idadi inayotakiwa ni Wanachama Mia Moja (100) au idadi isiyopungua nusu ya wajumbe wote.

## Dondoo Na. 4

### KUAFIKI DONDOO ZA MKUTANO

Kuafiki dondoo za Mkutano Mkuu.

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa kuafiki dondoo za Mkutano Mkuu kama zilivyowasilishwa.






Katibu mkuu Ndug. Godfrey Gerald Mweli akikabidhi cheti cha usajili wa Co-operative Bank of Tanzania (CBT) kwa Mwenyekiti wa Bodi Prof. Gervas Machimu.

# Dondoo Na. 5

**UWASILISHAJI WA CHETI CHA USAJILI CHA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA LIMITED.**

Co-operative Bank of Tanzania Limited ilisajiliwa rasmi tarehe 26 Mei 2024 baada ya kuungana kwa Kilimanjaro Cooperative Bank Limited na Tandahimba Cooperative Bank Limited.

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa kupokea Cheti cha Usajili cha Co-operative Bank of Tanzania Limited.



**BW. Godfrey Joel Ng'urah**
Mtendaji Mkuu

"Kwa hakika imekuwa ni mwaka wa mageuzi ya kitaasisi, kurejesha imani ya wateja, wadau na wanahisa kwaBenki yao. Kwa pamoja tumekusanya mtaji toshelevu kujenga uhimilivu na uendelevuwa Benki, ujumuishi wa kiuchumi na hatimaye kuanzisha Benki ya Ushirika Tanzania kwa ustawi wa pamoja wa wanahisa wetu, wateja wetu na wadau wa sekta ya ushirika nchini. Kwa yote haya ninayofuraha kubwa kuleta kwenu taarifa ya mafanikio makubwa ya mchakato na Uelekeo wetu kimkakati kwa miakamitano ijayo 2025 - 2029

Pamoja Tumeweza

# Dondoo Na. 6


**WASILISHO LA MPANGO MKAKATI WA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA LIMITED**

**Kinachohitajika**

Wanahisa wanaombwa kupokea na kujadili Wasilisho la Mpango Mkakati wa Co-operative Bank of Tanzania Limited.




## Mageuzi na Mwelekeo wa Kimkakati 2025-2029
## Ujumuishi wa Kifedha. Ustawi Kwa Wote



### Yaliyomo

1. Safari, Uzoefu na matokeo ya
2. Ushirika- Mtazamo wa Dunia/EA Tanzania
3. Ushirika Tanzania- Na Benki ya Ushirika.
4. Mikakati na Mbinu za Kibiashara 2025-2029
5. Matarajio ya Kifedha na Viashiria vyaMafanikio
6. Mikakati Endelevu na Ufadhili wa Mazingira (ESG)



# Safari Yetu, Uzoefu na Mageuzi Thabiti 2020-2024

**UZOEFU, MAGEUZI NA MATOKEO**

**MIKAKATI NA MATARAJIO**

**SAFARI YA MAGEUZI....HATUA KWA HATUA**

**WANAHISA KCBL/TCBL WAAMUA- NYAKATI MUHIMU YA SAFARI YETU**

- 2018 Bodi na Mkutano Mkuu wa Wahahisa waridhia Mageuzi ya Uendeshaji na Ukusanyaji Mtaji kwa kuruhusu Sekta binafsi kuwa sehemu ya Wamiliki na Wanaushirika
- 2020 Bodi na Mkutano Mkuu wa KCBL waidhinisha uwekezaji wa Kiimkakati wa CRDB Bank kwa ombi la SERIKALI
- Dec, 2021 , Mkutano Mkuu wa KCBL na TFC waidhinisha kuhamisha Fedha zilizokuwa TFC Kwenda KCBL kuanzisha Benki ya Ushirika
- 2022/23 Mikutano mikuu ya KCBL na TACOBA za ridhia na mchakato wa Kuanzisha Benki ya Ushirika kwa Kuungana
- 2024 KCBL na TCBL za ungana na kusajiliwa kama Benki ya Ushirika. Ukusanyaji mtaji waonyesha mafanikio makubwa na Benki mpya ushirika –CBT yapewa leseni na Benki kuu (BOT) na Mkutano mkuu wa Kwanza FGM wafanyika Dodoma

# Safari: Hali Halisi ya KCBL/TCBL -2020

Upotevu wa Fedha za wana hisa/Mtaji halisi- 8.3Bn

Limbikizo la Hasara Akiba ya wanahisa TZS 14.1Bn

Ukosefu wa kanuni, miongozo na sera bora za uendeshaji na Usimamizi wa Benki

Madai zaidi ya Bilioni 1 na Amana 6Bn a wateja zisizolipika kwa sababu ya Ukosefu wa Ukwasi

Mikopo Chechefu zaidi ya Bilioni 5, zaidi ya 95% ya Kitabu cha Mkopo

kwasi hasi ya -3.8% ambayo ni chini ya kiwango hitajika ya 20% hadi Kiwango hasi-3.8%

Mfumo Mama wa Benki na Miundombinu ya mawasiliano iliyopitwa na wakati

Sera na sheria za Ushirika zisizoshindani kwa huduma za kibenki

Muundo dhaifu wa Usimamizi na Uendeshaji

Wafanyakazi wengi wasio na Ueledi na ujuzi sahihi wa kibenki

Salio la Kitabu cha Mikopo cha TZS.276Mn baada ya kutafa mikopo Chechefu

## Mageuzi na Viashiria Vya Mafaniki 2020-2024o


## Viashiria Vya Matokeo Chanya: 2020-2023

| VIASHIRIA VYA UTENDAJI KUANZIA 2020 HADI DEC 2023 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S/N | VIASHRIA-KPI | MDA | | | | |
| | | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | UKUAJI |
| 1 | Faida baada ya kodi | (630) Milion | 293 Milioni | 327 Milioni | 489 Milioni | 187% |
| 2 | Mtaji halisi wa wanahisa | 2.2 Bilion | 2.74 Bilioni | 4.40 Bilioni | 14.1 Bilioni | 541% |
| 3 | Mikopo kwa wateja | 320 Million | 4.6 Bilioni | 7.5 Bilion | 8.7 Bilion | 2619% |
| 4 | Amana za wateja | 5.3 Milion | 5.4 Bilioni | 5.9Bilioni | 9.2 Bilioni | 74% |
| 5 | Mikopo chechefu | 74% | 3% | 2% | 3% | -96% |
| 6 | Jumla ya Mali | 8.5 Bilioni | 8.4 Bilioni | 11.5 Bilion | 25.9 Bilion | 205% |

CBT
Co-operative Bank



# Mafanikio Zaidi: Benki Bora kwa Umahiri na Weledi Tanzania 2023






# Mafanikio Zaidi: Benki Bora kwa Umahiri na Weledi Tanzania 2023







# 02

## Mtazamo na Uzoefu wa Benki za Ushirika Duniani/ Tanzania

## Uchumi wa Dunia/Tanzania

Uchumi wa Tanzania Umebakia Imara na Himilivu licha ya Changamoto za Kiuchumi Duniani



**Uchumi wa Dunia**

- Uchumi Duniani unakuwa kwa kasi ndogo, Mfumuko wa Bei na Riba zilizo juu toka Benki kuu za Serikali ya Marekani
- Katika Sekta ya Mabenki duniani, uwepo wa riba zilizo juu za serikali inapunguza ukwasi sokoni na uwezo wa wateja kurejesha Mikopo yao kwa wakati



**Uchumi wa Tanzania**

- Uchumi umebakia imara na Matarajio chanya ya ukuaji wa uchumi mpaka kufika GDP ya 5.6 % kufikia Q1 2024, ikichagizwa na uwekezaji na biashara duniani. Ni matarajio yetu Uchumi wa Tanzania utabakia imara na kukua kwa miaka 5 ijayo kufikia GDP ya 6% YoY
- Uhaba wa fedha za kigeni na kuyumba kwa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni unaongeza ghrama za huduma na upatikanaji wa bidhaa
- Ongezeko la Riba kwa sera za kifedha za Benki Kuu unaongeza gharama za mikopo iliyokopwa kwa fedha za kigeni

# Benki za Ushirika Duniani

**Soko na Wahusika**

Kulingana na World Cooperative Monitor (WCM) report ya 2023, vyama vikubwa vya Ushirika 300 viko ulaya.. Kati ya hizo 28 ni mabeeki ya Ushirika. Kama yanaonekana hapa kulia kulingana na mauzo yao kwa mwaka




Kulingana na European Association of Cooperative Banks (EACB) ripoti ya mwaka 2021, inaonyesha Benki kubwa ulaya kulingana na matokeo yao ya kifedha ya 2020.
Kulingana na Ripoti hiyo Benki kubwa 3 Ulaya za Ushirika zote ziko Ufaransa:
1.Credit Agricole,
2.Credit Mutuel
3 BPCE.
Hata Hivyo Benki na vyama vingine vikubwa vya Ushirika ziko Nertherlands, Belgium, South Korea, Japan, UK, USA, India na Canada

## Masomo Muhimu Kwa CBT : Uzoefu wa Dunia/Nchini

**Uzoefu wetu wa mageuzi kwa miaka 3 na uchambuzi wa mwenendo wa uchumi wa dunia na wa Tanzania unachagiza mambo makubwa matatu (3) ya kuzingatia tunapojipanga kimkakati kukabili siku za usoni za Benki yetu mpya ya Ushirika-CBT**

| | Viashiria Muhimu | Masomo/Uzoefu |
|---|---|---|
| I | Majanga na Viatarishi Duniani | • Kujenga uwezo mkubwa wa Kitaasisi, ubia na Mashirikiano<br>• Kujenga Uthabiti wa kimfumo kukabili mabadiliko yasiyokoma , dharura, majanga na teknolojia haribifu na bunifu<br>• Kujenga Misingi ya Utawala bora na Usimamizi |
| II | Ongezeko la Udhibiti wa Sekta ya Fedha | • Ongezeko la Gharama za kuendesha mabenki, Utawala bora na Imara wa sekta ya Fedha, Kudhibiti Vihatarishi Kimkakati na ulazima wa Kutekeleza Miongozo na sera ya Kisekta |
| III | Uwekezaji katika Mifumo ya Tehama na Kidijitali | • Kukubali na Kuitikia Mabadiliko ya kiteknolojia kwa Haraka<br>• Uthabiti na Utayari kupokea na Kujenga Benki ijayo ya Kidigitali |

--------CBT Strategy Review --------


## Mtazamo wa Dunia: Benki za Ushirika ni Tofauti: Uendelevu, Ukaribu, Uthabiti na Uhimilivu


Kulingana na ripoti ya Muungano wa Benki za Ushirika Ulaya (EACB 2021) , Benki za Ushirika zina modeli za kibiashara Tofauti zilizojengwa katika misingi ifuatayo:

| Misingi na Utofauti | Modeli na Falsafa za Benki za Ushirika Duniani |
|---|---|
| I Mwanachama/Mwanahisa ni Mteja | Wanahisa/Wanachama sio tu wamiliki ni Soko la kwanza na kubwa la wateja kwa Benki yenyewe |
| II Misingi ya Utawala Bora | Baada ya Mdororo wa Kiuchumi wa mwaka 2008- na Mabenki mengi kuanguka, Dunia na makampuni yalifunza na kuigiza misingi ya utwala bora (Uwazi, uwakilishi, ukweli, usawa, ueledi na heshima kwa wote) |
| III Ukaribu na Mahusiano Endelevu | Benki za Ushirika vinaamini katika ukaribu na mahusiano ya muda mrefu tofauti |
| IV Uthabiti/Uhimilivu | Benki nyingi za Ushirika ni thabiti na himilivu kwa sababu ya mitaji na akiba za wanachama ambazo ufanya vihatarishi vya soko kuwa chini na kukabili majanga. Kwa mfano Rabo Bank, ilipata AAA rating licha ya GFC ya 2008/2009 |
| V Ustawi na Matokeo Chanya kwa Jamii | Benki za Ushirika umilikiwa na wanachama ambao ndio pia wateja wake, uweka mkazo mkubwa kwenye falsa ya maadili na ustawi wa jamii ili kuwa na matokeo chanya kwa watu |

--------CBT Strategy Review --------

## Uzoefu wa Afrika Mashariki : Co-op Bank of Kenya



## Uzoefu wa Afrika Mashariki: Co-op Bank Kenya




## Masomo na Uzoefu Toka Co-op Bank of Kenya (1/3)

**Mifumo Thabiti ya Utawala Bora na Usimamizi**

**Uongozi mathubuti na misingi ya utawala bora ni siri ya mafanikio**

**Uwepo wa Mpango Mkakati Jumuishi na Shirikishi kwa biashara ya muda mrefu**

**Ni Muhimu CBT kuwa na Dira thabiti na Shirikishi ya Kufanya Biashara kwa muda mrefu**

**Mkazo na Rasilimali kubwa kwenye mageuzi ya Tehama na kidijitali**

**91% ya miamla zote ufanyika nje ya tawi na CBT lazimiwa iwekeze kwenye mifumo mbadala ya Kidijitali**

**Mawanda Mapana ya Bidhaa na Huduma**

**Bidhaa nyingi zinazoendana na mahitaji na aina ya wateja na sekta husika**

## Masomo na Uzoefu Toka Co-op Bank of Kenya (1/3)

**Mkazo kwenye Tehama na Mfumo mkuu mama wa Kibenki (CBS)**

**Uwekezaji kwenye Mifumo Jumuishi ya Kitaasisi Kukabiliana na Majanga, Viatarishi na dharura**

**Mkazo mkubwa kwenye Uendelevu/ESG na ufadhili wa miradi ya kimazingira**

> Mikopo zaidi ya dola 1 Million kati ya mikopo dola 294 Million ni ya kufadhili mazingira sawa na (33%) na mikopo ya maendeleo ya jamii (67%).

**Mteja/Wanachama Kwanza kwa kila uamuzi wa Kibiashara**

## Masomo muhimu na Uzoefu Toka Co-op Bank of Kenya (1/3)


**Mifumo Jumuishi ya Utoaji Huduma ( Matawi, Mawakala, ATM, Simu, Vituo vya Mauzo/malipo**

**Ubia na Mashirikiano ya Kimkakati na SACCOS/ AMCOS na Chama kikuu Hodhi cha Vyama vya Ushirika (CHC) kulinda maslahi ya Coop Bank of Kenya miongoni mwa Wanaushirika**




# Ushirika Tanzania na Benki ya Ushirika -CBT

Ushirika wa Fedha Tanzania-SACCOS 2023



Co-operative Bank

| VYAMA | WANACHAMA |
|---|---|
| 6000+ | 8 Millions+ |

**Kwa kutumia Idara yetu ya Tehama na Ubunifu , Benki ya Ushirika Tanzania (CBT) itashirikiana na Vyama vikuu, AMCOS, TFC na TCDC kufanya mageuzi na Ubunifu ili kuwezesha vyma kujiendesh Kidigitali na kuharakisha Ujumuishi wa Kifedha Nchini kwa zaidi ya watu milioni 10 ndani ya miaka 5 ijayo**

Ushirika Tanzania– Fursa na Changamoto

## Fursa

- **Vyama vilivyosajiliwa na wanachama kwenye mifumo Rasmi ya MUVU na Tume ya Ushirika –TCDC/TFC**
- **Vyama vina uongozi, utawala na umiliki wa Rasilimali vitu na watu**
- **Mashirikiano na ubia na serikali, tassisi za uthibiti na Wadau wa maendeleo ya sekta kama TCDC, BOT, WRRB, AGITF, TADB, CRDB,**
- **Fursa ya kuanzisha huduma na bidhaa za kidijitali kwa wanaushirika**
- **Fursa ya ujumuishi wa kifedha na kujipambanua kama Benki ya umma kwa wote (Economies of Scale)**
- **Soko Kubwa la Ushirika na wadau wake na mnyororo wa thamani wa kilimo biashara**
- **Fursa ya kuanzisha Vitengo bunifu vya kidijitali na huduma mbadala kwa wanaushirika**
- **Uwepo wa soko la watu binasfi na Fursa ya wadau, SMEs, MSEs, wasafirishaji na Wagavi**
- **Fursa ya kutanua bidhaa na njia za mapato kwa vyama na huduma mbadala kwa wateja**

## Changamoto

- **Changamoto ya usimamizi na utawala bora ndani ya Vyama**
- **Changamoto za kisheria na utamaduni wa kiushirika**
- **Mfumo na falsa ya maamuzi ya Kiushirika**
- **Uhaba wa Rasilimali watu wenye weledi na ujuzi**
- **Muingiliano wa Kisiasa**
- **Ushindani toka mabenki makubwa ya kibiashara kama CRDB na NMB**
- **Mahitaji yanayobadilika ya walaji na uwezo wa kitaasisi kubadilika**

# Fursa ya Mnyororo wa Thamani Katika Ushirika




## TOFAUTI KIUSHINDANI/CBT -NA BENKI ZINGINE ZA BIASHARA

1. Kuwa Benki Mwamvuli na Shindani kwa wanaushirika kwa biashara ya kibenki na Miamala ya kiushirika/Sekta
2. Kupanua wigo na fursa za uwekezaji kwa vyama vya Ushirika kushiriki fursa za uchumi mpana wa Taifa-Miradi ya kimkakati, Ajenda 10/30 na njia mbadala za uwekezaji
3. Kuchagiza Ushirika Kujiendesha kibiashra kwa kuongeza njia mbadala za mapato, ufanisi na tija ikiwemo gawio kwa vyama vya Ushirika
4. Kutoa huduma yenye gharama shindani nafuu kwa falsafa ya Biashara ya Jumla na Benki ya umma (Mass Banking on economies of scale)
5. Kutoa bidhaa bunifu za kifedha zinazokidhi mahitaji wateja na sekta ya Ushirika, wateja na wadau kwenye sekata ya ushirika
6. Kukuza ujumuishi wa kifedha kwa vyma, wakulima na makundi maalum ya kijamii na mnyororo wa thamani katika ushirika wakilimo na biashara

## Benki ya Ushirika-CBT ni Benki ya Biashara kwa Umma inayomilikiwa na Wanaushirika kwa wingi (Majority)

**Benki mpya ya Ushirika –CBT, Sio Benki ya Serikali ya Kilimo-bali ni Benki shindani ya kibiashara inayomilikiwa na vyama vya Ushirika- 51% na sekta Binafsi na Serikali -49% ili kuchagiza ukuaji wa Sekta ya kilimo na Ujumuishi wa Kifedha nchini**





# Mikakati na Matarajio 2025-2029


## Mwelekeo wa Kimkakati: 2025 hadi 2029


**Kukuza miundombinu ya Kibiashara, Ujumuishi wa kifedha ili kuongeza Tija ya uwekezaji wa fedha za wanahisa isiwe chini ya 14% ifikapo 2029**

| | |
|---|---|
| **Makusudi ya Uwepo wetu** | Kuchagiza mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa kuwezesha na kutoa huduma jumuishi za kifedha kidijitali ili kuboresha ustawi wa maisha ya watu wetu |
| **Maono Yetu** | Kuwa Benki Kiongozi ya Ushirika inayotoa bidhaa na huduma jumuishi za Kifedha |
| **Dhima Yetu** | Kutoa bidhaa na suluhisho la kifedha linalokidhi mahitaji ya wanachama na wateja wetu kwa kuzingatia ubunifu na teknolojia, ujumuishi wa kifedha, na uzoefu Chanya kwa wateja wetu ili kuongeza thamani ya uwekezaji kwa wadau na wanahisa. |



Vipaumbele na Maeneo ya Kimkakati- 2025-2029






# Matarajio ya Kifedha na Viashiria vya Mafanikio

Co-operative Bank

# Budgeti: 2025-2029

Tumejiwekea malengo ya Kimkakati kukuza mapato yetu na Faida ya Benki mwaka hadi mwaka kufikia 2029, kama inavyoonyesha hapa chini

MAPATO NA MATUMIZI

| Amounts in TZS Millions | | | Previous Year | Current Conso | Projections CBT Bank | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IS | TACOBA | KCBL | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 | 2027 | 2028 | 2029 |
| Interest Income | 555 | 1,630 | 2,185 | 3,688 | 8,021 | 13,069 | 18,711 | 24,988 | 33,096 |
| Interest Expenses | (85) | (140) | (224) | (383) | (1,976) | (3,784) | (5,675) | (7,597) | (9,652) |
| **Gross Financial Spread** | **471** | **1,490** | **1,960** | **3,305** | **6,044** | **9,285** | **13,037** | **17,390** | **23,444** |
| Non Interest Income | 259 | 326 | 585 | 653 | 5,922 | 9,386 | 13,150 | 17,374 | 22,018 |
| **Operating income** | **730** | **1,816** | **2,545** | **3,958** | **11,966** | **18,670** | **26,186** | **34,765** | **45,462** |
| Staff Expenses | (213) | (529) | (742) | (1,320) | (4,095) | (5,280) | (6,137) | (7,149) | (8,425) |
| Other Operating Expenses | (456) | (816) | (1,273) | (2,461) | (3,699) | (4,391) | (4,825) | (5,275) | (5,936) |
| **Total Other Expenses** | **(670)** | **(1,345)** | **(2,015)** | **(3,781)** | **(7,794)** | **(9,671)** | **(10,962)** | **(12,423)** | **(14,362)** |
| **Result before allowances** | **60** | **470** | **530** | **177** | **4,172** | **8,999** | **15,224** | **22,341** | **31,101** |
| Loan Impairment charges | 14 | (11) | 3 | (122) | (1,737) | (3,340) | (5,043) | (6,827) | (7,486) |
| Provision Other Assets | - | - | - | - | (6) | (8) | (10) | (12) | (14) |
| **Operating Result** | **74** | **459** | **533** | **55** | **2,429** | **5,651** | **10,172** | **15,502** | **23,601** |
| Recovery | 21 | - | 21 | 25 | 50 | 100 | 150 | 200 | 250 |
| **Profit before income tax** | **94** | **459** | **554** | **80** | **2,479** | **5,751** | **10,322** | **15,702** | **23,851** |
| Income Tax | (28) | (36) | (64) | (24) | (744) | (1,725) | (3,096) | (4,711) | (7,155) |
| **Net Profit after Tax** | **66** | **423** | **489** | **56** | **1,735** | **4,026** | **7,225** | **10,992** | **16,696** |

# Budgeti: 2025-2029

Tumejiwekea malengo ya Kimkakati kukuza Mizania ya Benki mwaka hadi mwaka hadi kufikia 2029, Ili kuwa na uwezo wa kukuza biashara

MIZANIA

| Amounts in TZS Millions | Audited 2023 | | Previous Year | Current Conso | Projections CBT Bank | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BS | TACOBA | KCBL | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 | 2027 | 2028 | 2029 |
| Cash & Balances with BoT | 263 | 2,225 | 2,488 | 2,350 | 7,992 | 16,632 | 26,352 | 37,152 | 49,032 |
| Balances with Other Banks | 1,567 | 5,805 | 7,371 | 9,271 | 9,500 | 8,700 | 8,300 | 9,500 | 10,500 |
| Government Securities | - | 6,209 | 6,209 | 23,490 | 33,210 | 36,810 | 40,860 | 45,360 | 55,260 |
| Loans & Advances | 2,854 | 8,762 | 11,617 | 15,274 | 63,874 | 126,514 | 196,984 | 275,284 | 374,284 |
| Other asset | 503 | 2,820 | 3,323 | 8,223 | 11,077 | 14,261 | 16,838 | 19,615 | 22,692 |
| **Total assets** | **5,188** | **25,821** | **31,009** | **58,609** | **125,653** | **202,917** | **289,334** | **386,911** | **511,768** |
| Total customer Deposit | 1,718 | 9,328 | 11,046 | 12,599 | 66,599 | 138,599 | 219,599 | 309,599 | 408,599 |
| Borrowings | 800 | - | 800 | 2,600 | 10,000 | 7,000 | 5,000 | 2,000 | 1,000 |
| Other Liabilities | 333 | 186 | 519 | 403 | 350 | 627 | 819 | 404 | 566 |
| Total Liabilities | 2,851 | 9,514 | 12,365 | 15,602 | 76,949 | 146,226 | 225,418 | 312,003 | 410,165 |
| Total capital | 2,336 | 16,308 | 18,644 | 43,007 | 48,704 | 56,691 | 63,916 | 74,908 | 101,603 |
| **Total Liabilities & Capital** | **5,188** | **25,821** | **31,009** | **58,609** | **125,653** | **202,917** | **289,334** | **386,911** | **511,768** |

# Viashiria na Vipimo vya Malengo 2025-2029

**Viashiria - Ukuaji wa Biashara**

| KPI Metric | 2025 | 2026 | 2027 | 2028 | Target (2029) |
|---|---|---|---|---|---|
| Capital (TZS Millions) | 48,704 | 56,691 | 63,916 | 74,908 | 101,603 |
| PAT (TZS Millions) | 1,735 | 4,026 | 7,225 | 10,992 | 16,696 |
| Loans and Advances (TZS Millions) | 63,874 | 126,514 | 196,984 | 275,284 | 374,284 |
| Deposits (TZS Millions) | 66,599 | 138,599 | 219,599 | 309,599 | 408,599 |
| NFI (%) | 49% | 50% | 50% | 50% | 48% |
| Branches | 6 | 8 | 9 | 10 | 12 |
| Agency Centers | 250 | 450 | 650 | 850 | 1,000 |

**Key KPIs – Operational Efficiency**

| Metric | 2025 | 2026 | 2027 | 2028 | Target (2029) |
|---|---|---|---|---|---|
| NPL | 3.4% | 3.3% | 3.2% | 3.1% | 2.5% |
| Efficiency Ratio | 65% | 52% | 42% | 36% | 32% |
| Return on Equity | 4% | 7% | 11% | 15% | 16% |
| Loan TAT Personal (Days) | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| LOAN TAT SME (Days) | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 |

**Key KPIs – Service Excellence**

| KPI Metric | 2025 | 2026 | 2027 | 2028 | Target (2029) |
|---|---|---|---|---|---|
| Active customer per segment | 70% | 70% | 70% | 70% | 70% |
| Net Promoter Score | 80% | 80% | 80% | 80% | 80% |
| System Uptime | 99.9% | 99.9% | 99.9% | 99.9% | 99.9% |
| Staff Retention | 95% | 95% | 95% | 95% | 95% |
| Process and Service Touchpoints Automation | 50% | 70% | 100% | 100% | 100% |




# Mashirikiano, Uendelevu, Mazingira na Utawala bora (ESG)

# Ubia Na Mashirikiano Kwa Uimara Na Uendelevu Wa Benki



UBIA NA SERIKALI, USHIRIKA JOINT ENTERPRISES –(UJE)

- **Kuimarisha Mahusiano ya Karibu na Serikali kwa kushirikiana na TCDC na Wizara ya Kilimo, ili Kuendeleza miradi ya Kimkakati na Kilimo biashara**
- **Kushirikiana Kimkakati na Chama mwamvuli wa uwekezaji wa Vyama vya Ushirika kwenye Benki ya CBT –Ushirika Joint Enterprises-(UJE) ili ku kulinda maslahi na biashara ya Ushirika kwa Benki ya Ushirika.**
- **Kushirikiana na Benki ya CRDB kimkakati katika kubadilishana utaalam, uzoefu, ujuzi, mifumo ya kibenki na utawala bora**

## Mikakati ya Uendelevu/Sustainability Strategy-ESG



**Kufadhili Miradi ya Kimazingira**

Kuzingatia madhara ya kimazingira kwa kila mradi/mkopo unaotolewa

Kuwa na sera ya miradi na utaoji mikopo inayozingati mazingia

Kushirikiana na wadau wa mazingira duniani kuounguza hewa ya Ukaa

**Kuimarisha utawala bora na Kudhibiti Viatarishi ndani ya Benki**

Kuwa na Sera na miongozo ya utawala bora kwa uendelevu na uwajibikaji

Miongozo na Sera za kudhibiti viatarishi

**Kurejesha kwa Jamii**


Benki Kurudisha kwa jamii angalu 1% ya Faida yake
Kufadhili Miradi yenye matokeo Makubwa kwa Jamii
Kuwekeza kwa vijana, Watoto na miradi yenye manufaa kwa jamii

**MIKOPO YA MAZINGIRA**

- Wanamazingira
- Viwanda na wazalishaji
- Kilimo Hai
- Kuifadhi Mazingira
- Kupanda Miti
- Kupunguza Hewa ya Ukaa
- Wafadhili

**WADAU**

- CBT
- AMCOS
- UNION
- TCDC
- SACCOS
- CRDB/WRRB/
- SERIKALI
- WAKULIMA
- WAKOPESHAJI




# AHSANTENI!

## Dondoo Na. 7

**KUPITISHA KATIBA (MEMARTS) YA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA LIMITED**

Randama ya Katiba ya Co-operative Bank of Tanzania

**Utangulizi**

Katiba ya Kampuni (Memorandum and Article of Association) ni hati au nyaraka za kisheria ambayo hutayarisha wakati wa usajili na uundaji wa kampuni kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2022. "Article of Assocaition" inasimamia masuala ya ndani ya uendeshaji wa kampuni na "Memorandum of Association" inahusu masuala ya nje ya kampuni. Katiba ya Kampuni ni nyaraka ya kisheria inayounganisha kampuni na wanahisa wake. Pia, ni mkusanyiko wa taarifa za kisheria na masharti ya kampuni ambayo yote kwa pamoja yanatoa mwongozo wa namna kazi za kampuni zinapaswa kufanyika pamoja na mgawanyo wa hisa kwa majina.

**"Memorandum of Association"**

'Memorandum of Assocition' inafafanua uhusiano wa kampuni na wanahisa na kubainisha malengo ya biashara na shughuli zitakazofanywa na Kampuni. Hati hii inasehemu kuu tisa (9) ikiwa ni pamoja na:

(i) Jina la kampuni kuwa ni Co-operative Bank of Tanzania.
(ii) Hadhi ya kampuni kuwa ni kampuni ya umma.
(iii) Ofisi ya kampuni kuwa ni Mkoa wa Dodama ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(iv) Malengo ya Kampuni.
(v) Majina, anwani, idadi ya hisa na sahihi za wanahisa.

**"Articles of Association"**

**"Articles of Association"** inafafanua taratibu na kanuni mbalimbali za uendeshaji na usimamizi wa kampuni. Pia, inaeleza kuhusu kumbukumbu za fedha na taarifa kuhusu kazi muhimu ambazo kampuni inalenga kuzifanya. "Articles of Association" inavipengele 156 ikiwa ni pamoja na:

**Tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika**
Jina la Kampuni ya Benki: "Co-operative Bank of Tanzania Public Limited Company"

**Ofisi ya Kampuni ya Benki:** Ofisi ya Kampuni itakuwa katika Mkoa wa Dodoma ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Malengo ya Kampuni:** Malengo ya "Co-operative Bank of Tanzania Public Limited Company" ni pamoja na:

(a) kufanya biashara ya benki katika matawi yake yote, wakala na idara zake zote, ikijumuisha kupokea fedha kutoka kwa umma kwa ujumla kupitia amana, dhamana, cheti, noti au dhamana nyingine, na kutumia fedha hizo, kwa ujumla au sehemu, kwa mikopo au uwekezaji;
(b) kutoa huduma za kibenki za kibinafsi, za ushirika, za kibiashara na za kifedha kupitia njia za kibenki za kitamaduni na njia za kisasa kupitia vyombo vya kielektroniki kama vile benki ya mtandao, uhamishaji wa pesa za kielektroniki kwenda na kutoka kwa matawi ya Benki, benki husika, vituo vya mauzo, na kiotomotela; kutoa miamala ya benki ndani na nje ya nchi, kutoa bidhaa kama vile taarifa ya benki mtandaoni, miamala ya akaunti, miamala ya kadi, mtandao na huduma za benki kwa njia ya simu, huduma za malipo ya bili za kielektroniki kupitia vifaa vilivyounganishwa au visivyotumia waya kama vile simu za mkononi, paja, wasaidizi wa kibinafsi wa kidijitali, kompyuta au vifaa vingine vinavyoweza kutoa muunganisho wa kieletroniki;
(c) kumiliki na kuendesha mashine za kiotomotela za kupokea na kulipa pesa ndani na nje ya nchi, kufanya kama watoaji wa kadi kwa kadi ya benki na kadi ya mkopo na kuwa wakala wa watoa kadi wengine ndani na nje ya nchi;

(d) kufadhili au kuwekeza katika kuendeleza mali miliki, hakimiliki, hataza, chapa, zinazohusiana na biashara ya benki na njia ya utoaji wa huduma za benki na bidhaa kwa ufanisi, haraka na gharama nafuu mbinu na mji na kuwa na uwezo wa kulinda dhidi ya watumiaji bila ruhusa na wavunjaji juu ya haki hizo, na

(e) kununua na kuuza sarafu za ndani na nje ya nchi.

**Mtaji na mgawanyo wa hisa:** Mtaji wa benki ni TZS. 100,000,000,000 uliogawanywa katika hisa 200,000,000 kwa thamani ya TZS. 500 kila hisa moja.

**Majina na mgawanyo wa hisa:** Majina na mgawanyo wa hisa ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapa chini.

| **Na.** | **Majina** | **Idadi** |
|---|---|---|
| 1. | Vyama vya ushirika | 51% |
| 2. | CRDB | 20% |
| 3. | Serikali | 10 |
| 4. | Watu binafsi, taasisi na kampuni | 19% |

**Mikutano ya Kampuni:** Kampuni itakuwa na Mikutano mikuu ya mwaka, mikutano mikuu ya kawaida mikutano mikuu ya dharura, mikutano ya maalumu pamoja na mikutano itakayoitishwa na wanahisa. Pia, inaonesha ajenda zitakazojadiliwa kwenye mikutano hiyo.

**Wakurugenzi:** Wakurugenzi pamoja na haki zao pamoja na namna ya kuwaondoa. Pia, muundo wa bodi ya wakurugenzi na upatikanaji wa wajumbe 12 wa bodi kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapa chini.

| Na. | Maelezo | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Vyama vya ushirika | 5 |
| 2. | CRDB | 2 |
| 3. | Serikali | 1 |
| 4. | Watu binafsi, taasisi na kampuni | 2 |
| 5. | Wakurugenzi huru | 2 |

## Dondoo Na.7

Aidha, namna ya kuwaondoa wakurugenzi, uchaguzi wa mwenyekiti wa bodi. Upatikananaji wa mkurugenzi mkuu, Katibu na mwenyekiti wa bodi umefafanuliwa.

**Gawio na Mfuko wa Akiba:** taratibu za kulipa wa gawio kwa wanahisa na haki ya kampuni kutumia gawio ambalo halijadaiwa kwa kipindi cha miaka 12 tangu kutolewa kwake imefafanuliwa.

**Akaunti na ukaguzi wa kampuni:** utunzwaji wa vitabu vya akaunti, mizania ya akaunti ya faida na hasara. Pia, taratibu za kuwapata wakaguzi na kuwapa haki ya kuwasilisha ripoti za ukaguzi katika mikutano mikuu umefafanuliwa.

**Hitimisho**
Katiba ya Co-operative Bank of Tanzania inayopendekezwa imegusia maeneo yote muhimu ambayo yanapaswa kuanishwa kiufasaha kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002.

**Mapendekezo/Maazimio**

a) Kuidhinisha randama ya Katiba ya Co-operative Bank of Tanzania (CBT).
b) Kukasimisha majukumu ya kukamilisha usajili wa kampuni kwa Bodi ya CBT

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa Kuidhinisha randama ya Katiba ya Co-operative Bank of Tanzania (CBT).
Wanachama wanaombwa kuidhinisha majukumu ya kukamilisha usajili wa kampuni kwa Bodi ya CBT.

## Dondoo Na. 8

**KUJADILI NA KUPITISHA MUUNDO WA USIMAMIZI WA UWEKEZAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA.**

**Pendekezo la kuanzisha chombo/taasisi itakayomiliki 51% ya hisa kwa niaba ya vyama vya ushirika kwenye benki ya Co-operative Bank of Tanzania (CBT)**

### 1.0 Utangulizi

Co-operative Bank of Tanzania Limited (CBT) imetokana na muunganiko wa vyama viwili vya ushirika vya Tandahimba Cooperative Benki Limited na Kilimanjaro Co-operative Benki Limited kwa mujibu wa Kifungu cha 96(1) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015. Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mamlaka aliyokabidhiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 77(2) ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015 aliisajili CBT kwa Namba ya Usajili AFF-DOM-DOM-CC-2024-108 kuanzia tarehe 26 Mei 2024.

Tarehe 10 Juni, 2024 CBT iliomba leseni ya benki ya biashara kwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT). BOT kupitia barua yake ya tarehe 23 Julai, 2024 iliridhia maombi ya CBT na kutoa leseni ya mpito yenye masharti kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaslisha Katiba ya CBT (Memorandum and Article of Assocaition (MEMART) kabla ya kuanza shughuli.

Kufuatia hali hiyo, CBT iliandaa randama ya Katiba kwa ajili ya kuisajili CBT kama Kampuni ya Umma (public company limited shares) kwa Mamlaka ya Usajili wa Kampuni na Leseni (BRELA). Randama ya Katiba iliyoandaliwa imezingatia mambo yafuatayo:

(a) Maamuzi ya wanahisa wa CBT kuhusu kuendesha benki kama kampuni waliyatoa kupitia Mikutano Mikuu ya mwaka 2018, 2019 na 2021.
(b) Kuweka mfumo jumuishi wa kiumiliki kwa kuwajumuisha wadau wengine wasiokuwa wanaushirika wanaomiliki 49%.
(c) Kuweka umiliki wa CBT kulingana na hisa kwa makundi yote yaani 51% ya vyama vya ushirika, 20% ya CRBD, 10% ya Serikali, na 19% ya taasisi/kampuni na watu binafsi.

### 2.0 Lengo la kuanzisha chombo/taasisi

Lengo la kuanzisha chombo/taasisi ni umiliki wa 51% wa hisa kwa niaba ya vyama vya ushirika pamoja na kuzifunga hisa hizo ili zimilikiwe na vyama vya ushirika peke yake. Pia, kulinda umiliki wa vyama vya ushirika na kutopoteza malengo ya uanzishaji wa CBT. Aidha, 51% ya hisa za vyama vya ushirika zitauzwa/kuhamishwa kwa vyama vya ushirika peke yake.

Timu ya Wataalamu ya Menejimenti kwa kuzingatia umuhimu wa kuanzisha chombo/taasisi ilimshirikisha Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kukubaliana kuwahusisha maafisa wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa ajili ya kupata uzoefu na maoni yao juu ya chombo/taasisi sahihi itakayoundwa kwa ajili ya kumiliki 51% ya hisa kwa niaba ya vyama vya ushirika.

Timu ya Wataalamu ya Menejimenti na maafisa wa TCDC walifanya kikao kazi kwa siku mbili kuanzia tarehe 8 hadi 9 Oktoba, 2024 katika Hoteli ya Midland Jijini Dodoma na kukubaliana kuwa “Joint Enterprise” ndicho chombo sahihi cha kumiliki 51% wa hisa za vyama vya ushirika kwa kuwa inajumuisha vyama vya ushirika vya ngazi zote.

Hivyo basi, ilikubalika kuwa CBT (ushirika) baada ya kukamilika kwa usajili wa kampuni, na kuhamisha mali na madeni kwenda CBT (kampuni) itabadilishwa na kuwa “Joint Enterprise”. CBT (ushirika) haitafungwa baada ya kuhamisha mali na madeni isipokuwa itabaki na vyama vya ushirika baada ya kuwaondoka watu binafsi, taasisi

na kampuni. Ili kufanikisha hayo mabadiliko ya kisheria na kiutendaji yanatakiwa kufanyika, ikiwa pamoja na masharti, jina, malengo na fungamano. Yafuatayo ni mabadiliko yanayopendekezwa kufanyika:

(a) Jina Name: Ushirika Joint Enteprises Limited (UJE)
(b) Fungamano: Vyama vya Ushirika vya ngazi zote (primary, secondary, middle level, union and federation)
(c) Malengo:
(i) Kumiliki uwekezaji kwa niaba ya vyama vya ushirika 51% ya hisa kwenye benki.
(ii) Kufanya uwekezaji mwingine kwa manufaa ya wanachama.
(iii) Kufanya uzengezi ili kuwezesha vyama vyote nchi kununua hisa kwa lengo la kuongeza uwekezaji wa vyama kwenye banki.
(iv) Kufanya uzengezi ili kuwezesha vyama vyote nchini vinafanya biashara na benki kwa ajili ya kuongeza faida na kuifanya benki kuwa shindani na enedelevu.
(v) Kutoa mafunzo na ushauri elekezi katika maeneo ya uwekezaji na fedha kwa wanachama.

**3.0 Vyanzo vya mapato**

(i) Gawiwo kutokana na uwekezaji ikiwa pamoja na 51% ya hisa za CBT.
(ii) Michango ya mwaka na ada ya uanachama.
(iii) Mapato kutoka na mafunzo na ushauri elekezi.
(iv) Vyanzo vingine vya mapato kama itakavyoelezwa na masharti ya chama.

**4.0 Muundo wa UJE: Muundo wa UJE utakuwa kama ifuatavyo:**

(i) Mkutano Mkuu ambao utakuwa na uwakilishi kutoka katika Kanda saba zikazoanzishwa ambazo ni (Dar es Salaam, Southern, Kaskazini, Magharibi, Lake, Kati na Nyanda za Juu). Kila Kanda itawakilishwa na mwakilishi mmoja katika Mkutano Mkuu wa UJE.
(ii) Mkutano Mkuu wa Kanda utachagua mwakilishi wa Mkutano Mkuu wa UJE na Wajumbe wa Bodi kama itakavyofafanuliwa kwenye masharti.
(iii) Mikutano Mikuu ya Kanda utakuwa wa uwakilishi kutoka kwenye vyama katika kanda husika. Mikutano Mikuu ya Kanda itachagua mwakilishi wa Mkutano Mkuu wa UJE na Mjumbe wa Bodi ya UJE.
(iv) Mkutano Mkuu wa UJE utachagua wawakilishi katika Mkutano Mkuu na wajumbe wa bodi wa CBT.

**5.0 Namna ya kuibadilisha CBT (ushirika) kuwa UJE**

CBT (ushirika) itahamisha mali na madeni kwenda CBT (kampuni). Hivyo, CBT (ushirika) itakuwa haina mali na madeni. Wanachama wa CBT (ushirika) watabaki kuwa walewale bila mali halisi kwa kuwa mali na madeni yatakuwa yamehamishiwa CBT (kampuni). Kuhamisha mali na madeni hakufuti uwanachama wa wanachama ndani ya CBT (ushirika).

CBT (ushirika) na wanachama wataendelea kubaki na wanaweza kukubaliana kubadilisha malengo na namna ya kupata fedha kwa ajili ya kuendesha CBT (ushirika). Ufuatao ni utaratibu wa kuibadilisha CBT (ushirika) kuwa UJE:

(a) Kufanya Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuridhia mabadiliko kwenda UJE kwa lengo la kumiliki 51% kwa niaba ya vyama vya ushirika.
(b) Kurekebisha masharti ya CBT (ushirika) ili yaendane na malengo ya uanzishaji wa UJE na jina jipya.
(c) Kufanya maboresho ya daftari la wanahisa ili kuwaondoa watu binafsi, taasisi na kampuni.
(d) Kuomba usajili wa UJE kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

### 6.0 Ufadhili kutoka CBT

CBT kwa ajili ya kulinda maslahi ya UJE, fursa za kiashara na kuiwezesha UJE kufanya shughuli zake kwa maslahi ya wanachama wake ipasavyo, inapendekezwa kuwa CBT ifadhili shughuli za uendesaji za UJE kama vile mkutano mkuu, bodi na menejimenti baada ya kusajiliwa. CBT na UJE watasaini mkataba wa ufadhili kwa ajili hiyo. Utaratibu wa ufadhili wa shughuli za msingi wa UJE unaopendekezwa kuwa mwaka wa kwanza 100%, mwaka wa pili 50%, mwaka wa tatu 25% na kuanzia mwaka nne UJE itajitegeme kwa 100%.

### 7.0 MAPENDEKEZO/MAAZIMIO:

c) Kubadilisha CBT kuwa Ushirika Joint Enterprises kwa kifupi UJE (51%) baada ya kusajili kuhamisha mali na madeni kwenda kwenye kampuni.
d) Kubadilisha masharti ya CBT (ushirika) na kuwa masharti ya UJE
e) Kukaimisha majukumu ya kukamilisha mchakato wa mabadiliko kwa Bodi ya CBT.

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa kujadili na kupitisha Muundo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Vyama vya Ushirika .

## Dondoo Na. 9

**KUIDHINISHA THAMANI NA MGAWANYO WA HISA KWA WANAHISA WAANZILISHI WA CO-OPERATIVE BANK OF TANZANIA LIMITED.**

**Hesabu ya hisa mpaka kufikia 30 septemba 2024**

| NA. | TAARIFA | NAMBA YA HISA | BEI KWA HISA | THAMANI YA HISA | NAMBA YA WANAHISA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TCBL | 2,762,265 | 500 | 1,381,132,500 | 2,222 |
| 2 | KCBL | 41,450,469 | 500 | 20,725,234,500 | 2756 |
| 3 | Ambazo hazija tambuliwa | 106,130.00 | | 53,065,015 | 43 |
| | **Total** | **44,318,864** | | **22,159,432,015** | **5,021** |

| NA. | TAARIFA | NAMBA YA HISA | BEI KWA HISA | THAMANI YA HISA | NAMBA YA WANAHISA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Jumla ya Hisa kwa KCBL na TCBL | 44,318,864 | 500 | 22,159,432,000.00 | 5,021 |
| | **Total** | **44,318,864** | | **22,159,432,000.00** | **5,021** |

Hadi tarehe 30 Septemba 2024, kwa Pamoja benki ina jumla ya hisa zipatazo 50.6Mn, hata hivyo bado kuna hisa 106,130 hazijaweza kutambuliwa ni nani hasa aliweka fedha. Kwa kuzingatia ukosekanaji wa taarifa kwa hisa hizo, kwa madhumuni ya ripoti hii, kiasi hicho kimetambuliwa kama kwa idadi ya miamala ambayo ni 43 katika taarifa ya wanahisa, uongozi wa benki bado wanaweka juhudi zaidi kufanya utambuzi Zaidi wa hisa hizo.

## TAARIFA ZA MTAJI WA KCBL KUFIKIA 30 SEPTEMBA 2024

| MAELEZO | KIASI | KIASI |
|---|---|---|
| Mtaji kabla ya Uwekezaji wa CRDB | | 5,423.00 |
| Watu binafsi na Taasisi zingine | 1120 | |
| Vyama vya Ushirika | 4303 | |
| Uwekezaji kutoka kwa wawekezaji wapya | | 15,355.30 |
| Watu binafsi na Taasisi zingine | 7280.05 | |
| Vyama vya Ushirika | 8075.25 | |
| Mtaji kutoka kwa wawekezaji wapya | | |
| Jumla ya Uwekezaji wa KCBL | | 20,778.30 |

Dondoo Na. 9

## TAARIFA ZA MTAJI WA TCBL KUFIKIA 30 SEPTEMBA 2024

| MAELEZO | KIASI | KIASI |
|---|---|---|
| Mtaji uliolipwa | | 1,381.00 |
| - Tandahimba District Council | 632 | |
| - Cooperatives (AMCOS & TANECU) | 355 | |
| - CRDB Bank | 100 | |
| Watu binafsi na Taasisi zingine | 294 | |
| Hifadhi ya Mtaji | | |
| | | |
| Jumla ya Uwekezaji wa KCBL | | 1,381.00 |
| | | |
| | | |

## Dondoo Na. 9

## MTAJI JUMUISHI KATI YA KCBL NA TCBL KUFIKIA 30 SEPTEMBA 2024

| DESCRIPTION | AMOUNT | PERCENTAGE |
|---|---|---|
| Mtaji uliolipwa | | 22,159 |
| Watu binafsi na Taasisi zingine | 9,326 | |
| Vyama vya Ushirika | 12,733 | |
| - CRDB Bank | 100 | |
| Jumla ya Mtaji | | 22,159 |

## MGAWANYO WA HISA KUFIKIA 30 SEPTEMBA 2024

| MCHANGANUO | KIASI "000,000" | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Vyama vya Ushirika | 26,520 | 51% |
| CRDB Bank | 10,400 | 20% |
| Watu binafsi na Taasisi nyingine | 9,880 | 19% |
| Serikali | 5,200 | 10% |

Hata hivyo, vyama vya Ushirilka bado vina upungufu wa Tsh. 8.8 Bilioni ili kufikia adhma ya vyama vya Ushirikia kumiliki 51%

**Kinacho hitajika**

Wanachama wanaombwa kuidhinisha thamani na mgawanyo wa hisa kwa wanahisa waanzilishi wa Co-operative Bank of Tanzania Limited.

## KUDHINISHA UKOMO WA MADENI KWA MWAKA 2024

### 1.0 Utangulizi

Cooperative Bank of Tanzania (CBT) ina mpango wa kukuza biashara na vitabu vya mikopo katika mkakati wake wa kufikia makundi mbalimbali ya Ushirika na wasio Wanaushirika katika jamii ya Watanzania. Mpaka kufikia Septemba 30, 2024 benki ilikuwa imetoa mikopo ya Shilingi Bilioni 14 kwa makundi mbalimbali katika soko ikiwa ni pamoja na vyama vya Ushirika, Wakulima, Wajasiriamali, Vijana na Wanawake.
Kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 benki imepanga kukuza kitabu cha mikopo hadi kufikia Shilingi Bilioni 63 sawa na ukuaji wa asilimia 350. Ongezeko hili la mikopo vilevile utaongezea benki mapato yatokanayo na riba. Ukuaji huu utachagizwa na ongezeko la matawi, wateja, huduma zilizoboreshwa kwa wateja na bidhaa zilizobuniwa ili kuongeza thamani na faida kama ilivyo katika mpango wa muda mrefu wa benki 2025-2029.

### 2.0 Lengo la Mkopo

Menejimenti ya Benki inatarajia kukopa kiasi cha Shilingi Bilioni 10.0 kutoka katika taasisi za kifedha kwa kipindi cha mwaka 2024/2025. Lengo la mkopo ni kuongeza ukwasi wa benki hivyo kuwa na uwezo wa kutoa huduma za mikopo kwa wateja wengi zaidi katika sekta mbali mbali ikiwemo Vyama vya Ushirika.

### 3.0 Dhamana ya Mkopo

Benki itajadiliana na taasisi za kifedha katika soko ili kupata riba rafiki, vigezo na masharti ya ulipaji. Mkopo utadhaminiwa na hati fungami zilizopo BOT na akaunti za muda maalumu zilizopo katika benki zingine.

### 4.0 Urejeshaji wa Mkopo

Kulingana makubaliano na taasisi za fedha, mkopo huu utalipika kwa kipindi kisichozidi miezi 36.

### 5.0 Pendekezo

Bodi na Menejimenti inaomba Wanahisa kupokea, kujadili na kuidhinisha pendekezo la Ukomo wa madeni wa Shilingi Bilioni 10.0 kutoka taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) kuwezesha biashara ya benki ya kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika, Wajasiriamali, Wafanyakazi wa Umma na Wafanyabiashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 6.0 Kinachohitajika

Wanachama wanaombwa kuidhinisha mkopo wa shilingi bilioni 10.0 kutoka taasisi za fedha ikiwemo Benki ya kilimo Tanzania (TADB) kuwezesha biashara ya benki ya kutoa mikopo kwa Vyama vya Ushirika, wajasiriamali, wafanyakazi wa umma na wafanyabiashara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Salamu;



Prof. Gervas Machimu,
**MWENYEKITI WA BODI**

# Dondoo Na. 11

## KUIDHINISHA MKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA 2024/2025

### Utangulizi

Co-operative Bank of Tanzania Limited (CBT) ni benki iliyoundwa baada ya kuunganisha Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) na Tandahimba Co-operative Bank Limited (TCBL). Benki hiyo ilianza shughuli zake mwezi Oktoba 2024.

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha (BFIA), 2006 na kanuni zake, Benki inatakiwa kuwa na mkaguzi wa nje. Uteuzi wa mkaguzi wa nje unawasilishwa kwa mkutano mkuu wa wanahisa kulingana na BAFIA na kanuni zake.

Benki kwa mujibu wa sheria tajwa hapo juu ilitangaza zabuni shindani kwa ajili ya uteuzi wa Mkaguzi wa nje kwa CBT kwa robo ya mwisho ya mwaka utakaomalizika 31Desemba 2024 na kwa mwaka utakaoishia tarehe 31 Desemba 2025. Makampuni matatu ya ukaguzi yalionyesha nia ya kutoa huduma za ukaguzi wa nje kwa CBT ambayo yaliwasilishwa kwenye kikao cha Bodi kwa ajili ya mapendekezo kwenye Mkutano Mkuu kuidhinisha uteuzi wa Mkaguzi wa nje.

**Pendekezo**
Kulingana na uzoefu na gharama za ukaguzi, Bodi inapendekeza kwa Mkutano Mkuu kumuidhinisha INNOVEX AUDITORS, wa S.L.P 75297, DAR ES SALAAM kuwa Mkaguzi wa nje kwa mwaka 2024 na 2025 kwa ada ya jumla ya TZS 36,431,320.00.

Naomba kuwasilisha.



Prof. Gervas Machimu,
MWENYEKITI WA BODI

**Kinachohitajika**
Wanachama wanaombwa kupitisha azimio la kumuidhinisha INNOVEX AUDITORS, wa S.L.P 75297, DAR ES SALAAM kuwa Mkaguzi wa nje kwa mwaka 2024 na 2025 kwa ada ya jumla ya TZS 36,431,320.00.

**PENDEKEZO LA KUPOKEA MALI NA MADENI KUTOKA TANDAHIMBA COOPERATIVE BANK LIMITED NA KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED**

**Pendekezo**

Tandahimba Cooperative Society Limited na Kilimanjaro Co-operative Society Limited vilivyopewa leseni ya kufanya biashara ya benki na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa mujibu wa Kifungu cha 96(1) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015
.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mamlaka aliyokabidhiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 77(2) ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015 aliisajili CBT kwa Namba ya Usajili AFF-DOM-DOM-CC-2024-108 kuanzia tarehe 26 Mei 2024. Aidha, tarehe 10 Juni, 2024, CBT iliomba leseni ya benki ya biashara kwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT). BOT kupitia barua yake ya tarehe 23 Julai, 2024 iliridhia maombi ya CBT na kutoa leseni ya mpito yenye masharti mbalimbali na kuagiza yatekelezwe kabla benki haijaanza shughuli zake.

TCBL na KCBL kupitia Mikutano Mikuu yao iliyofanyika tarehe 19.03.2024 na 28.07.2023 mtawaliya iliridhia kuhamisha mali na madeni kwenda CBT baada ya kusajiliwa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika.

Kufutia hali hiyo, TCBL na KCBL kwa nyakati tofauti walithaminisha mali zao kwa ajili ya kupata thamani halisi ya mali na madeni kabla ya kuhamishia CBT. Jedwali hapa chini linafafanua zaidi mali na madeni yanayohamishiwa CBT:

| TAASISI | MAELEZO | THAMANI (TSHS) |
|---|---|---|
| KCBL | **MALI** | |
| | Mali zinazohamishika, Jengo na kiwanja | 2,521,489,385.59 |
| | Mali zisizohamishikika | 214,680,104.21 |
| | Mikopo (409) | 10,872,911,686.82 |
| | Mali nyingine | 757,399,962.58 |
| | Hati fungani | 10,517,642,471.99 |
| | Fedha taslimu na zilizopo Benki kuu ya Tanzania | 1,979,873,968.66 |
| | Salio na Uwekezaji katika Taasisi zingine za kifedha | 5,466,583,216.93 |
| | Mikataba mbalimbali | 29 |
| | Idadi ya Kesi zilizopo Mahakamani 10. Kati ya hizo 2 KCBL inadai jumla ya TShs. 3,357,331,866.00 | 3,357,331,866.00 |
| | MADENI NA MTAJI | |
| | Madeni Mengine | 2,347,902,534.44 |
| | Jumla ya akaunti 16917 zikiwa na jumla ya amana za wateja | 10,267,791,051.67 |
| | Mtaji wa wanahisa | 19,714,887,291.42 |

## Dondoo Na. 12

| TAASISI | MAELEZO | THAMANI (TSHS) |
|---|---|---|
| | **MALI** | |
| TCBL | Mali zisizohamishika | 63,706,234.20 |
| | Mali zinazohamishika | 307,105,094.65 |
| | Mikopo (577) | 3,397,011,820.75 |
| | Fedha taslimu | 262,626,400.00 |
| | Salio na Uwekezaji katika Taasisi zingine za kifedha | 371,741,184.50 |
| | Mali nyingine | 628,532,184.90 |
| | Madeni Mengine | 1,349,346,752.60 |
| | Akaunti (12956) | 1,256,273,341.24 |
| | Mtaji wa wanahisa | 2,258,867,095.00 |
| | Idadi ya kesi zilizopo Mahakamani - Tano zenye jumla ya: | 244,338,730.40 |

**MAPENDEKEZO/MAAZIMIO:**

(i) Kupokea mali na madeni kutoka TCBL na KCBL na kuwa mali na madeni ya CBT kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali hapo juu.

(ii) Kukaimisha majukumu yaliyobaki ya kuhamisha mali na madeni ikiwa pamoja na kuhamisha mali na madeni kutoka CBT (ushirika) kwenda CBT (kampuni) kwa Bodi ya CBT.

## Dondoo Na. 12

**MAPENDEKEZO/MAAZIMIO:**

(i) Kupokea mali na madeni kutoka TCBL na KCBL na kuwa mali na madeni ya CBT kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali hapo juu.

(ii) Kukaimisha majukumu yaliyobaki ya kuhamisha mali na madeni ikiwa pamoja na kuhamisha mali na madeni kutoka CBT (ushirika) kwenda CBT (kampuni) kwa Bodi ya CBT.

**Kinachohitajika**

(i) Wanachama wanaombwa kupokea mali na madeni kutoka TCBL na KCBL na kuwa mali na madeni ya CBT kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali hapo juu.

(ii) Wanachama wanaombwa kukaimisha majukumu yaliyobaki ya kuhamisha mali na madeni ikiwa pamoja na kuhamisha mali na madeni kutoka CBT (ushirika) kwenda CBT (kampuni) kwa Bodi ya CBT.

## Bidhaa za Benki

## Dondoo Na. 13

**KUIDHINISHA KUHAMISHA MALI NA MADENI KUTOKA CHAMA KWENDA KAMPUNI.**

**Pendekezo**

Kupokea mali na madeni kutoka TCBL na KCBL na kuwa mali na madeni ya CBT kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali hapo juu.

**Kinachohitajika**

Wanachama wanaombwa kuidhinisha kuhamisha mali na madeni kutoka Chama Kwenda Kampuni.

## Dondoo Na. 14

### 1.0 Utangulizi

Co-operative Bank of Tanzania Limited (CBT) imetokana na muunganiko wa vyama viwili vya ushirika vya Tandahimba Cooperative Society Limited na Kilimanjaro Co-operative Society Limited kwa mujibu wa Kifungu cha 96(1) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015. Mrajis wa Vyama vya Ushirika kwa mamlaka aliyokabidhiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 77(2) ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015 aliisajili CBT kwa Namba ya Usajili AFF-DOM-DOM-CC-2024-108 kuanzia tarehe 26 Mei 2024.

Tarehe 10 Juni, 2024, CBT iliomba leseni ya benki ya biashara kwa Benki Kuu ya Tanzania (BOT). BOT kupitia barua yake ya tarehe 23 Julai, 2024 iliridhia maombi ya CBT na kutoa leseni ya mpito yenye masharti kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaslisha Katiba ya CBT (Memorandum and Article of Association (MEMART) kabla ya kuanza shughuli.

Kufuatia hali hiyo, CBT iliandaa randama ya Katiba kwa ajili ya kuisajili CBT kama Kampuni ya Umma (public company limited by shares) kwa Mamlaka ya Biashara na Leseni (BRELA). Pamoja na mambo mengine, randama ya Katiba iliyoandaliwa imeanisha idadi ya wajumbe wa Bodi na namna watakavyopatika.

Kanuni za Benki Kuu (the Banking and Financial Institutions (Corporate Governance Regulations, 2021), CBT inatakiwa kuwa na wajumbe wa bodi wasiopungua 12. Kati ya hao, wawili ni wajumbe huru na wawili wawakilishi wa wanahisa wenye hisa chache.

### 2.0 Muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ya CBT

Kwa mujibu wa Kanuni za Benki Kuu, randama ya Katiba ya Benki iliyoandaliwa na utawala bora, Bodi ya Wakurugenzi itajumuisha wajumbe wenye utaalamu katika masuala ya fedha, utawala, uhasibu, sheria, ushirika, Uchumi na mengineyo.

Muundo wa Bodi ya Wakurugenzi kutoka na kundi la wanahisa kwa mujibu wa Katiba ya Benki inayopendekezwa ni kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali kurasa ifwatayo:

| Na | Kundi la Wanahisa | Idadi wa Wajumbe wa Bodi |
|---|---|---|
| 1) | Vyama vya ushirika | 5 |
| 2) | Benki ya CRDB (CRDB Bank Plc) | 2 |
| 3) | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 1 |
| 4) | Wanahisa wenye hisa chache | 2 |
| 5) | Wakurugenzi Huru | 2 |

CBT inatarajiwa kuanza shughuli zake rasmi baada ya kusajiliwa kama Kampuni, hivyo ni vyema wanahisa kuchagua wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi sasa ili kuondoa ombwe la kisheria, kiutawala na kiuendeshaji. Pia, kuiwesha benki kuanza kufanya kazi bila mkwamo wowote.

Inapendekezwa kwamba jumla ya wajumbe wanne (4) wa Bodi (wawili wajumbe huru na wawili wajumbe wawakilishi wa kundi la Wanahisa wenye hisa chache) wachaguliwe na wanahisa katika Mkutano Mkuu huu ili kuungana na wajumbe wengine kutoka katika makundi mengine ya wanahisa yaliyoorodheshwa kwenye jedwali hapo juu ili kukamilisha muundo wa Bodi ya Wakurugenzi ya CBT baada ya kusajiliwa na kupewa leseni kamili na BOT.

MAAZIMIO/MAPENDEKEZO

(i) Kuridhia utaratibu wa uchaguzi ulioanishwa katika Katiba ya Kampuni utumike kuchagua wajumbe ili kupata uhalisia wa uwawikilishi kulingana idadi ya hisa.

(ii) Kuchagua wajumbe wanne (4) (wawili wajumbe huru na wawili wajumbe wawakilishi wa kundi la Wanahisa wenye hisa chache) kama inavyooneshwa hapa chini.

1. Dkt. Veronica Robert Nyahende
2. Dkt. Joseph Ochieng Witts
3. Bi Aikande Clement Kwayu
4. CPA Mwamini J Mussa
5. CPA Dkt. Saganga M. Kapaya
6. CPA Hillary Andrea Ngowi
7. Bw. Silvanus Benedict Mola
8. Bw. Suleimani Mayongela
9. Bw. Peter Situmbeko Nalitolela

John Rugambo
**Katibu wa Benki**

Godfrey Ng'urah
**Mkurugenzi Mtendaji**




# Taarifa wa Mkuu wa Fedha, Habari Teknolojia na Ubunifu, Mkuu wa CBT na Biashara



# TAARIFA YA KAIMU MKUU WA FEDHA

Kwa kipindi kinacho ishia 2024 ulikua ni mwaka wa mafanikio na ukuaji kwa benki yetu, ambapo mnamo tarehe 30.09.2024 taarifa ya fedha ya Pamoja inaonyesha benki ilifanikiwa kupata matokeo bora na chanye yenye kuonyesha nuru zaid katika kufanya vizuri zaidi kwa siku zijazo.

Benki ilifanikiwa kujiimarisha katika mizania yote muhimu ambapo Kwa mwaka wa fedha 2024, benki imefanikiwa kupata faida ya TZS. 646Mn, kitabu cha mikopo kimefikia TZS. 14.4Bn, amana za wateja zimerekodi TZS. 11.4Bn, na mtaji wa wanahisa umefikia TZS. 22Bn.

Na kwa sasa, Idara ya fedha na utawala imejiimarisha na kuhakikisha uendelevu wa mafanikio zaidi sambamba na kukuza mizania ya Benki na uwekezaji wa wanahisa.

## Viashiria MATOKEO CHANYA YA KIFEDHA : 2020 - 2024

| Namba | Viashiria - KPA | Septemba 24<br>Kiasi "000,000" |
|---|---|---|
| 1 | Faida kabla ya kodi | 605 |
| 2 | Mtaji halisi wa wanahisa | 22,086 |
| 3 | Mikopo kwa wateja | 14,439 |
| 4 | Amana za wateja | 11,414 |
| 5 | Mikopo chechefu | 2% |
| 6 | Jumla ya mali | 37,009 |
| 7 | Jumla ya mapato | 2,030 |

CPA . Kinyaki O . Kinyaki
**Kaimu Mkuu wa Fedha**

# TAARIFA YA KAIMU MKUU WAHABARI ,TEKNOLOJIA NA UBUNIFU



**Safari Mpya ya Benki ya Ushirika Tanzania Kidigitali**

Katika ulimwengu wa teknolojia na huduma za kifedha, ushirikiano na ubunifu ndio injini za maendeleo. Hii ni hadithi ya muungano wa kidigitali kati ya Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) na Tandahimba Co-operative Bank Limited (TCBL), Benki mbili ambazo zimeungana ili kuunda Co-operative Bank of Tanzania (CBT). Katika zama hizi za teknolojia ya kisasa, lengo letu ni kutoa huduma bora, za haraka, na zenye ufanisi kwa wateja wetu, tukitumia mifumo ya kidigitali na huduma za kiteknolojia kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wateja popote walipo.

Muungano huu umeongozwa na hitaji la kuunda mfumo wa kifedha wa kisasa, ambao utaunganisha huduma za matawi na huduma za kidigitali kama vile ATM, benki za mtandao, benki za simu, huduma za mawakala (agency banking), na benki za mkononi (mobile banking), na kuwapa wateja wetu uzoefu wa benki wa haraka na wa uhakika.

**Hatua Muhimu za Kidigitali Zilizofikiwa Hadi Sasa**

Katika mchakato wa kuunda Co-operative Bank of Tanzania (CBT), hatua za kiufundi zimechukuliwa ili kuhakikisha kuwa benki inakuwa tayari kidigitali na hizi ni baadhi ya hatua muhimu zilizofikiwa:

- **Muungano wa Mfumo wa Msingi wa Kidigitali (CBS):**
  Hatua muhimu imefikiwa kwa kuunganisha mifumo ya msingi ya KCBL na TCBL katika mfumo mmoja wa kisasa wa kidigitali. Uhamishaji wa data na taarifa za wateja ulifanyika kwa usalama, na sasa CBT inafanya kazi chini ya mfumo wa CBS uliounganishwa, ambao unawezesha miamala ya haraka zaidi na ya uhakika kwa wateja wetu.

- **Miamala ya Kati ya Matawi kwa Wakati Halisi (Real-Time):** Baada ya kuunganisha mifumo, CBT imeanza kutekeleza miamala ya wakati halisi kati ya matawi yote. Hii inamaanisha wateja sasa wanaweza kufanya miamala katika tawi lolote la CBT bila kujali tawi walilofungua akaunti.

- **Huduma za Kidigitali:** Huduma za kidigitali za CBT zimeimarishwa kupitia:

  - ATM: Mashine zetu za ATM zimeunganishwa na mfumo mpya wa CBS, hivyo miamala yote itakuwa ya haraka zaidi na yenye ufanisi.

  - Kila kitu mkononi (Mobile Banking): Wateja wetu wanaweza kufurahia huduma za benki kupitia simu zao za mkononi, zikiwa na urahisi wa kufanya miamala, kuangalia salio, kulipia bili, na kufanya uhamisho wa pesa kwa wakati halisi.

- Huduma za Mawakala (Agency Banking): Kupitia uhusiano uliopo na benki ya CRDB, wateja wanaweza kupata huduma za kibenki kwa haraka kama vile kutoa pesa, kuweka pesa, au kufanya miamala mingine ya benki kwa urahisi bila kutembelea matawi ya benki kupitia mawakala wote wa CRDB.

- **Uanzishaji wa Matawi Mapya ya Dodoma na Tabora:** Kama sehemu ya upanuzi wetu wa kidigitali, matawi hay yataongeza upatikanaji wa huduma zetu kwa wateja wa maeneo hayo. Matawi haya yataleta uzoefu wa kisasa wa kibenki kwa kutumia mifumo ya kisasa ya Tehama.

Kuimarisha Huduma za Kidigitali na Ubunifu
Tunapoendelea na safari hii ya kidigitali, hatua zifuatazo zimepangwa ili kuimarisha zaidi huduma za benki na kuhakikisha tunabaki mstari wa mbele katika ubunifu wa kiteknolojia:

- **Uchakataji wa Hundi (Cheque Clearing Automation):** Tutaanzisha mfumo wa motomatiki wa kusafisha hundi ambao utawezesha malipo ya hundi kushughulikiwa haraka na kwa uhakika zaidi. Hii itaharakisha mchakato wa hundi na kupunguza muda wa kusubiri kwa wateja.

- **Utekelezaji wa RTGS kwa Malipo ya Wakati Halisi (Real-Time Settlement):** Tutaanzisha huduma ya RTGS (Real-Time Gross Settlement) ambayo itawawezesha wateja kufanya malipo ya benki kwa benki kwa wakati halisi. Hii itarahisisha miamala ya kifedha kwa wateja wetu na kuhakikisha uwazi na usalama wa miamala ya interbank.

- **Kuimarisha Huduma za Kidigitali:** Benki itaendelea kuboresha huduma za kidigitali kama vile benki ya mtandao, benki ya simu, benki ya mkononi na huduma za mawakala. Hii itawawezesha wateja wetu kufurahia huduma za benki popote walipo, kwa njia rahisi na salama zaidi.

- **Benki ya Mtandao (Internet Banking):** Huduma hii inatoa njia rahisi na salama kwa wateja wetu kufanya miamala ya benki wakiwa popote duniani

- **Mafunzo Endelevu na Usaidizi kwa Wafanyakazi:** Wafanyakazi wataendelea kupokea mafunzo ya kiufundi na msaada ili kuhakikisha huduma bora kwa wateja wakati tunapojenga benki hii mpya. Mafunzo haya yatazingatia zaidi matumizi ya teknolojia mpya na mifumo ya kisasa.

Mustakabali wa Kidigitali wa Benki yetu.
Benki yetu inajivunia kuwa mstari wa mbele katika mapinduzi ya kidigitali ya benki nchini Tanzania. Muungano huu sio tu unaleta benki mbili pamoja, bali pia unaleta mustakabali bora wa huduma za kifedha kwa wateja wetu wote. Kwa kutumia teknolojia za kisasa, Benki yetu itakuwa ni Benki ya ushirika yenye nguvu, inayojali wateja wake, na inayotoa huduma bora za kisasa za kifedha zinazokidhi mahitaji ya ulimwengu wa kidigitali.

Safari hii ya muungano wa kidigitali ni mwanzo tu. Tukiwa na mifumo ya kisasa na malengo ya ubunifu, tutaendelea kuimarisha huduma na kuboresha uzoefu wa wateja wetu, tukizingatia thamani ya ushirikiano na teknolojia.

Hemed Nassor
**Kaimu Mkuu wa Kitengo Habari ,Teknolojia na Ubunifu**

# TAARIFA YA KAIMU MKUU WA MIKOPO



**Mafanikio Katika Mikopo**
Co-operative Bank of Tanzania (CBT) inajumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 14, baada ya kuunganisha mikopo kutoka Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) yenye thamani ya Shilingi 11.09 na mikopo kutoka Tandahimba Co-operatie Bank Limited (TCBL) yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.92.

Benki inampango wa kukuza biashara na vitabu vya mikopo katika mkakati wake wa kufikia makundi mbalimbali ya Ushirika na wasio Wanaushirika katika jamii ya Watanzania. Kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 benki inatarajia kukuza kitabu cha mikopo hadi kufikia Shilingi Bilioni 63 sawa na ukuaji wa asilimia 350. Ongezeko hili la mikopo vilevile utaongezea benki mapato yatokanayo na riba, kuboresha mizania ya benki ikiwa ni pamoja na ongezeko la mali za mda mrefu za Benki. Ukuaji huu utachagizwa na ongezeko la matawi, wateja, huduma zilizoboreshwa kwa wateja na bidhaa zilizobuniwa ili kuongeza thamani na faida kama ilivyo katika mpango wa muda mrefu wa benki 2025-2029.

Benki imeendelea kuthibiti mikopo chechefu na kufanya kuwa asilimia 3. Malengo ya Menejimenti ni kuwa na mikopo chechefu ya chini ya asilinia 2% hadi kufikia Desemba 2024. Ongezeko la mikopo chechefu limetokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya kiuchumi. Hata hivyo Menejimenti imefanya jitihada madhubuti na kufanikiwa kuongeza ubora wa mikopo kuwa asilimia 3% chini ya takwa na BOT la mikopo chechefu isiyozidi asilimia 5%. Tumeendelea kuboresha bidhaa zetu za mikopo kwa Vyama, Vijana, Vikundi, Wamama, Wakandarasi, Sekta ya Utalii na Wafanya biashara wengine. Bidhaa hizi hutolewa kwa riba nafuu ili kuwezesha kutoa huduma jumuishi za kifedha.

Frank S. Wilson
**Kaimu Mkuu wa kitengo cha Mikopo**

# TAARIFA YA MKUU WA BIASHARA NA USHIRIKA



**Mafanikio katika Biashara**

Co-operative Bank of Tanzania (CBT) inajumla ya amana zenye thamani ya Shilingi Bilioni 11.6, baada ya kuunganisha amana kutoka Kilimanjaro Co-operative Bank Limited (KCBL) zenye thamani ya Shilingi 10.4 na amana kutoka Tandahimba Co-operatie Bank Limited (TCBL) zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.2.

Mwaka 2024, ni mwaka "kujiimarisha kimkakati kupitia mabadiliko ya kimuundo wa Taasisi zetu mbili KCBL na TCBL ili kuongeza ufanisi zaidi wa kutoa huduma na bidhaa kwa wateja wetu" sambamba na kuifanya Benki yetu kuwa imara na shidani katika kutoa huduma na bidhaa zake. Baada ya kuunganisha KCBL na TCBL, Benki yetu ya CBT mpaka kufikia tarehe 30.09.2024 imefikia Jumla ya Wateja 29,873

Katika utekelezaji wetu wa mkakati wa Biashara wa miaka 5 . Menejimenti ya Benki imejipanga katika utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuzingatia maendeleo ya tehama. Benki imekwisha ongeza bidhaa za kidijitali ikiwa ni pamoja na huduma ya Benki kwa njia ya simu "Coop Mobile Banking" inayomwezesha mteja wa CBT kupata huduma za kibenki kupitia simu yake ya kiganjani popote . Aidha Benki iko mbioni kukamilisha bidhaa na huduma za kidijitali ikiwemo huduma ya Benki mtandao "Internet Banking" pamoja na huduma ya uwakala "agent banking".

CPB. Yahya Jumanne Kiyabo
**Mkuu wa kitengo cha Biashara na Ushirika.**


TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
TACOBA
"Our Bank for Our Development"
MKUTANO MKU
WANACHAMA
COOP ATIV
Ushirika wetu
Twende
Pamoja


Bens
Fungicide


Jiwezeshe
Account



**MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

## Dondoo Na. 16

**KUFUNGA MKUTANO**

Co-operative Bank of Tanzania Limited,
S.L.P 201, Dodoma, Tanzania